



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS –TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI NJOMBE



TAARIFA KWA UMMA

MAPOKEZI YA FEDHA SHILINGI 2,078,909,081.01 KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI

KWENYE SEKTA YA ELIMU NA AFYA.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe anapenda kuutaarifu umma kuwa Halmashauri ya Mji Njombe kwa Robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/2024 impokea fedha kutoka serikali kuu kiasi cha TSH. 2,078,909,081.01 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye sekta ya Elimu na Afya.

Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:

1. Halmashauri imepokea Shilingi Milioni 288.90 kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF kwa ajili ya :

Ujenzi wa Madarasa matatu (03) na nyumba za walimu (2in1) Shule ya msingi Boimbanda TSH. 87,937,295.29 ,Ujenzi wa nyumba ya waganga 2in1 katika zahanati ya Ikisa TSH.100,485,892.86 na Ujenzi wa Uzio katika zahanati ya Ikisa TSH. 100,485,892.86.

2. Idara ya Elimu Sekondari imepatiwa shilingi Milioni 232 kwa ajili ya :

Ujenzi wa Madarasa 3 Shule ya Sekondari Njombe (NJOSS) TSH.83,000,000.00,Ujenzi wa Madarasa 3 shule ya Sekondari Uwemba TSH. 75,000,000.00, Ujenzi wa Madarasa 2 Shule ya Sekondari Maheve TSH.50,000,000.00 na Ujenzi wa 12 V.I.P Pit latrine Shule ya Sekondari Matola TSH.24,000,000.00

3. Idara ya Elimu Msingi imepatiwa shilingi Milioni 208 kwa ajili ya :

Ujenzi wa madarasa 6 Shule ya Msingi Lunyanywi TSH. 50,000,000.00,Ujenzi wa madarasa 3 Shule ya Msingi Muungano TSH. 25,000,000.00,Ujenzi wa madarasa 2 Shule ya Msingi Mfereke TSH.50,000,000.00 ,Ujenzi wa madarasa 2 na ofisi 1Shule ya Msingi Chalima TSH.25,000,000.00,Ujenzi wa madarasa 2 na ofisi 2 katika Shule ya Msingi Kilenzi TSH.30,000,000.00,Ujenzi wa matundu 7 ya vyoo Shule ya Msingi Kitulila TSH.14,000,000.00 na Ujenzi wa matundu 7 ya vyoo Shule ya Msingi Itulike TSH.14,000,000.00.

4. Idara ya Afya ,Lishe na Ustawi wa Jamii imepatiwa Shilingi Bilioni 1.35 kwa ajili ya:

Ukarabati wa Hospital ya Halmashauri Kibena TSH. 900,000,000.00,Ununuzi wa Vifaa Tiba kituo cha afya Muungano (Kifanya) TSH. 150,000,000.00,Ununuzi wa Vifaa Tiba kituo cha afya Luponde TSH.150,000,000.00,Ununuzi wa Vifaa tiba katika Zahanati ya Madobole TSH.34,000,000.00,Ununuzi wa Vifaa tiba katika Zahanati ya Kihesa TSH.33,000,000.00,Ununuzi wa Vifaa tiba katika Zahanati Ngalanga TSH. 33,000,000.00 na ukamilishaji wa Zahanati ya Itipula TSH.50,000,000.00.

Imetolewa na:

Ichikael Malisa.

Afisa Habari.

Halmashauri ya Mji Njombe.